
# Songea yetu

MWEZI MACHI-2019

TOLEO NAMBA 1

MACHI 2019

Abdul Hassan Mshaweji
Mstahiki Meya Manispaa Songea



M/S Tina Sekambo
Mkurugenzi Manispaa Songea

YALIYOMO


- TATIZO LA MAJI KUBAKIA HISTORIA
- TASAF YABADILISHA MAISHA YA KAYA MASIKINI
- BARAZA LA MADIWANI LAPITISHA BAJETI YA BILIONI 41
- SERIKALI YATOA MILIONI 100 KUJENGA MADARASA
- HIFADHI YA ASILI YA LUHIRA ILIYOPO SONGEA
- IFAHAMU MANISPAA YA SONGEA
- MAPATO STENDI YA MFARANYAKI YAONGEZEKA KWA ASILIMIA 300
- MILANGO YA UTALII YAFUNGULIWA SONGEA
- WANAFUNZI SONGEA KUFUNDISHWA KIJIDITALI


## Tatizo la maji Manispaa ya Songea kubakia historia

TATIZO la maji katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma litabakia kuwa historia baada ya serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa kutoa kiasi cha zaidi ya Dola milioni 50 kwa ajili ya kutekeleza mradi mkubwa wa maji katika kata zote 21 na mitaa yote 95 iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea.Akizungumza katika Mkutano wa Baraza la madiwani la manispaa ya Songea,Mbunge wa Jimbo la Songea mjini na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki Dkt.Damas Ndumbaro amesema mradi huo unatekelezwa na nchi ya India na kwamba mradi unatarajia kuanza Septemba 2019.

Hata hivyo amesema hali ya upatikanaji wa huduma ya maji pembezoni mwa ya Songea ni asilimia 46.6



*Mbunge wa Songea Mjini Dkt.Damas Ndumbaro*

## Kituo cha Afya Ruvuma kukamilika Aprili 2019

MRADI wa ujenzi wa kituo cha afya Kata ya Ruvuma Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma ambacho serikali imetoa shilingi milioni 400 unatarajia kukamilika mwanzoni mwa mwezi ujao.

Kituo hicho kikikamilika kinatarajia kutoa huduma kwa wakazi zaidi ya 45,000 wanaoishi katika kata za Ruvuma,Subira,Mateka na majengo.

# TASAF ilivyobadilisha maisha Songea

Hawa Hassan(57) Mkazi wa mtaa Pachanne,kata ya Mjimwema anasema kabla ya kuanza kupata ruzuku ya shilingi 36,000 kutoka TASAF alikuwa anaishi katika mazingira magumu kwa kuwa mume wake alimuacha mara ya baada ya kupata maradhi ya miguu.

Amesema kutokana na ruzuku hiyo aliamua kuanza biashara ya ndogo ndogo ya kuuza mafuta ya kula na nyanya, na kucheza upato hivyo kufanikiwa kupata shilingi



Mume wa Hawa Hassan, Mzee Musa Ismali(67) amekiri ruzuku ya TASAF inawasaidia katika mambo mengi na kwamba hivi sasa mke wake ,anasumbu

liwa na maradhi ambapo fedha kiasi cha shilingi 250,000 ambayo imetokana na ruzuku ya TASAF ndiyo inayotumika katika matibabu yake na shughuli za kilimo. Afisa Mtendaji wa Mtaa wa PACHANNE Sophia Michael amesema katika Mtaa huo kuna jumla ya wanufaika wa TASAF 148

# Sekondari 4 Songea zapewa mil.100



Tina Sekambo Mkurugenzi wa Manispaa

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma Tina Sekambo amekiambia kikao cha Baraza la madiwani wa Halmashauri hiyo kuwa serikali imetoa shilingi milioni 100 katika shule 4 za sekondari ili kutekeleza mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa.Shule hizo ni sekondari ya Mateka,Msamala,Lizaboni na Matarawe.

**Manispaa ya Songea yazindua wiki ya wanawake**



UZINDUZI wa wiki ya wanawake duniani ambayo kilele chake ni Machi nane mwaka huu imezinduliwa na mgeni rasmi Meneja wa Benki ya posta Mkoani Ruvuma Albert Kombo ndani ya bustani ya Manispaa ya Songea mjini Songea.Kilele cha maadhimisho hayo katika Manispaa ya Songea kinatarajia kufanyika Namanditi Kata ya Ruhuwiko .

“Katika tukio la mashujaa hao kunyongwa walitimiza wajibu wao kwa ajili ya maslahi ya taifa letu la sasa na kizazi kijacho ambapo ushujaa ndiyo njia pekee ya kujikomboa na kuutangaza utalii wa kiutamadu’’,alisema

## Milango ya utalii Manispaa ya Songea yafunguliwa

AFISA Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma Afrikanus Challe anabainisha kuwa,wadau wa utalii katika Mkoa wa Ruvuma wamekusudia kuanzisha utalii wa kiutamaduni (cultural tourism) sanjari na kuboresha maeneo yote ya kihistoria ili kuendeleza utamaduni hatimaye maeneo hayo yaweze kuingiza mapato baada ya watalii kutembelea kama ilivyo katika visiwa vya Zanzibar.Challe anasema,wadau kutoka wilaya zote za mkoa wa Ruvuma tayari wameshatembelea maeneo muhimu ya kihistoria kama vile Makumbusho ya Taifa ya Majimaji, Maposeni,Luhira na Chandamali katika Wilaya ya Songea il

mashujaa hao wakiwemo mashujaa 68 ambao walinyongwa na kuzikwa katika kaburi moja.

“Katika tukio la mashujaa hao kunyongwa walitimiza wajibu wao kwa ajili ya maslahi ya taifa letu la sasa na kizazi kijacho ambapo ushujaa ndiyo njia pekee ya kujikomboa na kuutangaza utalii wa kiutamaduni



Ofisi za Manispaa ya Songea

## Miaka 114 ya mashujaa wa Majimaji

KILELE cha kumbukizi ya mashujaa wa Majimaji kimefanyika Februari 27 mwaka huu ndani ya Makumbusho ya Taifa ya Majimaji mjini Songea .Hapa ni moja ya vivutio vya utalii wa kishujaa ambapo ni kaburi la pamoja la mashujaa 66 ambao walizikwa humu mara baada ya kunyongwa na wajerumani kipindi cha vita ya Majimaji mwaka 1906.Shughuli rasmi za kuelekea kilele zilianza kuanzia Februari 25 na kuendelea mfululizo hadi siku ya kilele.Mkurugenzi wa makumbusho ya Taifa ya Majimaji Mhifadhi Kiongozi Batazar Nyamusya anasema maadhimisho ya mwaka huu yana hadhi ya kimataifa kwa sababu wamealikwa machifu toka nchi mbalimbali ziliwemo Afrika ya kusini,Cameroun,Malawi na Zambia.

Mgeni rasmi katika maadhimisho

# Luhira hifadhi ya asili iliyopo mjini Songea



Hifadhi ya asili ya Luhira iliyopo mjini Songea ni moja ya kivutio adimu cha utalii kilichopo kilometa saba toka mjini Songea mkoani Ruvuma. Hii ndiyo hifadhi pekee ya asili katika nchi nzima iliyopo mjini .Ina wanyama wa aina mbalimbali wakiwemo pundamilia, nyani,mbawala, kakakuona, aina 105 za uyoga, nyoka wa aina mbalimbali wakiwemo chatu na ndege wa aina mbalimbali . Hifadhi hii ilianzishwa mwaka 1973 .

Hifadhi ya Luhira ina ukubwa wa hekta 600.Licha ya hifadhi hiyo kuwa na wanyama wa aina mbalimbali wakiwemo pundamilia, pongo, fisimaji, nyani, tumbili, kakakuona, kobe na chatu. Tozo ya kiingilio Raia wa Tanzania watu wazima sh.2000,watoto wenye umri kati ya miaka sita hadi 16 sh.500 na Watoto chini ya miaka sita ni bure.

Sekta ya utalii katika Manispaa ya Songea imefungua milango ambapo hivi sasa vivutio vipya vya utalii vimeibuliwa na vya zamani vinatangazwa ili kuvutia watalii wa ndani na nje ya nchi. Miongoni mwa vivutio hivyo ni milima ya matogoro,Makumbusho ya Taifa ya Majimaji na Luira

***Hifadhi ya Luhira ina ukubwa wa hekta 600.Licha ya hifadhi hiyo kuwa na wanyama wa aina mbalimbali wakiwemo pundamilia, pongo, fisimaji, nyani, tumbili, kakakuona,***

## Mapato stendi ya Mfaranyaki yaongezeka kwa asilimia 300

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma Tina Sekambo amesema Halmashauri ya Manispaa hiyo imeanza kunufaika na mradi wa kituo cha mabasi cha Mfaranyaki ambapo ukusanyaji wa mapato umeongezeka kwa asilimia zaidi ya 300 na kwamba kodi ya vibanda pia imeongezeka toka kati ya shilingi 25,000 hadi 50,000 kwa mwezi hadi 250,000 hadi 300,000 kwa mwezi.

Sekambo amesema ongezeko hilo limetokana baada ya kufanyika ukarabati wa stendi hiyo ambao umefanya na Benki ya Dunia kupitia miradi ya ULGSP kwa gharama ya zaidi ya shilingi milioni 550.Amesema wajasirimali wakubwa na wadogo wamevutiwa kufanya biashara




# Songea yapitisha bajeti ya zaidi ya bilioni 41




BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma limefanya kikao maalum cha kupitisha bajeti ya Halmashauri katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 ambapo ,kikao hicho kimepitisha zaidi ya shilingi bilioni 41.


Akizungumza katika Kikao hicho Mwenyekiti wa kikao ambaye pia ni Mstahiki Meya wa Manispaa ya Songea Alhaj Abdul Hassan Mshaweji amesema wamejipanga kusimamia ukusanyaji wa mapato na kwamba hawatasita kuchukulia hatua mtumishi yeyote wa umma ambaye atabainika kuhujumu mapato ya Halmashauri .

“Tutakuwa wakali kwa watumishi watakaobainika kutafuna mapato ya Halmashauri,pia tumejipanga kuongeza vitega uchumi ”,alisisitiza.

Dira ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea ni kuwa kitovu cha uwekezaji na maendeleo ya viwanda ili kufikia maendeleo endelevu ya jamii 2025.

Manispaa ya Songea ina kata 21 na mitaa 95

# Vivutio vya milima ya Matogoro



Milima ya Matogoro

HAPA sio kilele cha Mlima Kilimanjaro bali ni kilele cha mlima Matogoro uliopo Manispaa ya Songea Mkoa wa Ruvuma wenye vivutio adimu vya utalii ambavyo bado havifahamiki na wengi.Mlima Matogoro ni chanzo mito mitatu ya Ruvuma,Luhira na Luegu. Kuna msitu mnene na eneo zuri la kufanyia picnic pamoja na vivutio lukuki ambavyo havipatikani

### Songea ina ziada ya chakula tani 40,000

HALI ya upatikanaji wa chakula katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma inaridhisha ambapo kuna jumla ya Hekta 24,340.8 ambazo zililimwa msimu wa 2016/2017 na kuzalisha tani 98,671.76. wakati mahitaji ya chakula ni tani 58,280 hivyo .

### Songea ina viwanda zaidi ya 500

HALMASHAURI ya Manispaa Songea ina jumla ya viwanda 512 kati ya viwanda hivyo kiwanda kikubwa ni kimoja viwanda vidogo ni 132 na viwanda vidogo sana ni viwanda 371.

# Machinjio ya kisasa ya Songea

*"Kukamilika kwa mradi huu kutaofanya manispaa yaSongea kuwa na machinjio bora zaidi Tanzania"*

Ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Songea katika Kata ya Tanga Manispaa ya Songea umefikia zaidi ya asilimia 95. Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya zaidi ya bilioni 3.2 na kwamba Kukamilika kwa mradi huu kutaboresha uchinjaji wa wa kisasa hivyo kuongeza ubora wa bidhaa za nyama. Mradi huu unajengwa chini ya programu ya uboreshaji wa miji na Manispaa (ULGSP).

Kukamilika kwa mradi huu kutaofanya manispaa yaSongea kuwa na machinjio bora zaidi Tanzania bara.



# Bustani ya Manispaa inavutia wengi



Bustani ya Songea mjini

UBORESHAJI wa bustani ya Manispaa ya Songea kupitia Mzabuni anayeendesha bustani hiyo,umeanza kuvutia wageni wengi wanaotembelea mji wa Songea .Uchunguzi umebaini idadi kubwa ya wageni inakuwa kubwa siku za sikukuu na mwisho wa wiki.Hata hivyo Mzabuni anaendelea na kazi ya uboreshaji ili kuhakikisha bustani hiyo inakuwa ya kuvutia na kubadilisha muonekano wa mji Songea.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhandisi Stella Manyanya amesema bustani imeujengea heshima mji wa Songea kwa kuwa wageni wengi wanaotembelea Mkoa wa Ruvuma wamepata mahali sahihi pa kupumzikia na kuburudika kwa michezo mbalimbali na vyakula .

Mradi huu umefadhiliwa na Benki ya Dunia kwa gharama ya zaidi ya shilingi milioni 399.

# Barabara za lami Songea zafikia asilimia 60

MRADI wa ujenzi wa barabara katika kiwango cha lami Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma umefikia asilimia 60 na unatarajia kukamilika Septemba 30,2019.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea Tina Sekambo amesema Ujenzi wa barabara kiwango cha lami km 10.3 katika barabara za kati kati ya Mji umeanza mwezi Machi, 2018 .

Anamtaja Mkandarasi aliyefuzu kujenga barabara hizo kuwa ni Kampuni ya SIETCO ya watu wa Jamhuri ya China na kwamba hadi kukamilika mradi huo utagharimu jumla ya Tshs. 10,960,078,230.00.

Barabara ta FFU Matogoro ujenzi wake umekamilika ambapo hivi sasa wananchi wananufaika.

Wakazi wa Matogoro sasa wameepukana na tope na vumbi ambalo lilikuwa kero



*''Barabara ta FFU Matogoro ujenzi wake umekamilika ambapo hivi sasa wananchi wananufaika na barabara hiyo''.*

## TALGWU Mkoa wa Ruvuma yazindua vitambulisho vipya

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) katika Mkoa wa Ruvuma kimezindua vitambulisho vipya kwa wanachama wake hai.Uzinduzi wa kimkoa umefanyika kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea kwa kugawa vitambulisho 460 kwa wanachama hai.Uzinduzi umefanywa na Mwenyekiti wa TALGWU Mkoa wa Ruvuma Willy Lwambano kwa kushirikiana na Katibu wa TALGWU Mkoa wa Ruvuma Ashraf Chussi.

Akizungumza katika hafla hiyo Katibu wa TALGWU Mkoa wa Ruvuma Ashraf Chussi amesema chama hicho kimeamua kutoa vitambulisho hivyo vya kisasa lengo likiwa ni kuhakikisha wanachama wake wanaingizwa kwenye mtandao ambao watafahamika katika nchi nzima.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa TALGHWU Mkoa wa Ruvuma Willy Lwambano amesema vitambulisho hivyo vinaweza kuwawezesha wanachama kukopa Benki


# Ifahamu Manispaa ya Songea

HALMASHAURI ya Manispaa ya Songea iliyopo mkoani Ruvuma, inakadiriwa kuwa na idadi ya Watu 252,150 wakiwemo Wanaume 119,182 na Wanawake 132,968 kutokana na ongezeko la asilimia 4.4 kwa mwaka, Aidha ina jumla ya Kaya 61,930 kwa wastani wa watu 4.2 kwenye kila kaya.

Halmashauri ina jumla ya Mitaa 95, Kata 21 na Tarafa 2. Halmashauri ina jumla ya waheshimiwa madiwani 28, kati yao 21 ni wa kuchaguliwa, 7 ni wawakilishi Viti Maalum. Halmashauri inalo jimbo moja la uchaguzi ambalo Mbunge wake ni Mhe. Damas Ndumbaro na Mbunge wa Viti Maalum Mhe. Jackline Ngonyani



Tina Sekambo Mkurugenzi



Mradi wa bustani ya Manispaa ya Songea uliofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa gharama ya shilingi milioni 399.Mradi huu upo jirani na Jengo la NSSF na Mkabala na Ofisi za Halmashauri ya Manispaa ya Songea ,barabara ya Sokoine mjini Songea.Mradi umeanza kazi na umeshaanza kuwanufaisha wakazi wa mji wa Songea.

# Habari katika picha



Mradi wa Machinjio ya kisasa ya Songea unaotekelezwa katika Kata ya Tanga kwa gharama ya shilingi bilioni 3.2.

Mradi huu hadi sasa umefikia zaidi ya asilimia 95 na hivi sasa upo katika hatua ya mwisho ya umaliziaji katika awamu ya kwanza.Machinjio hii inatarajiwa kuwa ya kwanza kwa ubora.

# Habari katika picha



Mradi wa kituo cha Afya Kata ya Ruvuma katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea ambao serikali imetoa shilingi milioni 400.
Mradi huu umefikia asilimia 80,Mradi unatekelezwa kwa kujenga majengo manne ambayo ni Jengo la Mama na Mtoto,Jengo la upasuaji,Huduma za wagonjwa wanne na jengo la maabara.

# Habari katika picha



Muonekana wa mradi wa ujenzi wa stendi ya kisasa ya mabasi katika eneo la Tanga Manispaa ya Songea kwa ufadhili wa Benki ya Dunia ambao unagharimu zaidi ya shilingi bilioni 10.

Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya wachina ya SIETICO kwa mkataba wa miezi 18,mradi huu ulionza Machi 2018,unatarajia kukamilika Septemba 30,2019.Mradi umefikia asilimia 54

# Habari katika picha



KATIKATI ni Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea Alhaj Abdul Hassan Mshaweji akifungua kikao cha Baraza la madiwani la Halmashauri ya Manispaa hiyo kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea mjini Songea.
Kulia kwa Mstahiki Meya ni Naibu Meya wa Manispaa ya Songea Judith Mbogoro na kushoto kwa Mstahiki Meya ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea Tina Sekambo

# Habari katika picha






Picha ya kwanza ni kaburi la pamoja la mashujaa wa 66 wa vita ya Majimaji walionyongwa na kuzikwa mwaka 1906 na picha ya pili ni kaburi la Jemedari wa wangoni Songea Mbano

***JARIDA HILI HUTOLEWA KILA MWEZI NA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA***

***BODI YA UHARIRI***

***1.TINA SEKAMBO***
***MKURUGENZI WA MANISPAA YA SONGEA***

***2.ALBANO MIDELO***
***AFISA HABARI MANISPAA YA SONGEA***

***HALMASHAURI YA MANISPAA***
***Anuani ya Posta: P O BOX 14, SONGEA***
***Simu ya Mezani: 025 2602970***
***Simu ya Kiganjani:***
***Baruapepe info@songeamc.go.tz***
***Tovuti:songeamc.go.tz***

## TANGAZO

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WA MANISPAA YA SONGEA KUJITOKEZA KWENYE USAFI WA MAZINGIRA KATIKA MITAA NA MAKAZI YAO JUMAMOSI YA MWISHO WA MWEZI MACHI,2019.

KUFANYA USAFI JUMAMOSI YA MWISHO WA MWEZI NI TAKWA LA KISHERIA,MNAOMBWA WOTE KUSHIRIKI

**Songeamc.go.tz**

# Wanafunzi Songea kufundishwa kidijitali

SHIRIKA la Kanisa katoliki la DONBOSKO Network limetoa vishikwambi 1824 ,kompyuta mpakato 38 na powepoint 19 katika shule kumi za msingi katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

Mhasibu wa DONBOSKO padre Celestine Kharkongor amesema vifaa hivyo vina thamani ya shilingi milioni 885 na kwamba lengo ni kuhakikisha walimu na wanafunzi wanatumia vifaa vya kieletroniki katika tendo la kujifunza na kufundisha na kuleta mapinduzi katika elimu.

Padre Celestine amesema mradi huu unafanyika katika awamu ya pili upande wa Zanzibar na wilaya Songea mkoani Ruvuma,mradi unatekelezwa katika Halmashauri za Manispaa ya Songea na Halmashauri ya wilaya ya Songea.Amesema DONBOSKO imetoa masanduku 35 yenye vishikwambi 96 kwa kilashule,power point na kompyuta mpakato katika shule za msingi zilizopo kwenye mradi,vifaa vyote vikiwa na thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 1.575.

Hata hivyo amesema awamu ya kwanza ya mradi huo ilianza mwaka 2017 katika shule za msingi katika mikoa ya Dodoma,Iringa,Dar es salaam,Kilimanjaro na Morogoro.

Kwa upande wake Padre Peter Mutechura ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika la DONBOSKO Network Tanzania anayeshughulikia Maendeleo na elimu amesema kupitia program hii mwalimu atatumia vifaa vya kijiditali kama jukwaa la kufundishia na kuifanya wilaya ya Songea kuingia katika mfumo wa kisasa wa kufundishia.

Afisa Elimu Msingi katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea Zakia Fandy amelishukuru shirika la DONBOSKO kwa kuanzisha mradi huo katika shule kumi za Manispaa ya Songea ambapo amesema hiyo ni fursa nyingine katika manispaa ya Songea.Hata hivyo amewaagiza walimu wakuu kuhakikisha mradi unatekelezwa kulingana na malengo yaliyowekwa na vifaa hivyo visitumike katika matumizi yasiyostahili.